**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

# CHUO CHA UALIMU WA UFUNDI STADI MOROGORO

## TANGAZO LA NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO

Mkuu wa Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro (MVTTC) anatangaza nafasi za kujiunga na Mafunzo ya kozi za Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi kwa mwaka wa masomo 2025/2026, Dirisha la Mwezi Machi, 2025.

### 1.0. Kozi za Mafunzo

### 1.1. Stashahada ya Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi (Ordinary Diploma in Technical and Vocational Teacher Education)–NTA Level 6

**Sifa za Kijiunga**

Muombaji awe na Stashahada ya Ufundi sawa na 'Ordinary Diploma' (NTA Level 6) au sifa linganishi zinazotambulika na Mamlaka za Urekebu na Ithibati.

**Muda wa Masomo**

Muda wa masomo kwa kozi hii ni Miaka Miwili (Miezi 24).

### 1.2. Cheti cha Walimu Wasaidizi wa Ufundi Stadi (Certificate of Assistant Vocational Teacher)

**Sifa za Kujiunga**

Muombaji wa kozi hii anatakiwa awe na:

i) Cheti cha Elimu ya Sekondari (CSEE) chenye ufaulu usiopungua masomo mawili, bila kujumuisha masomo ya dini, na

ii) Cheti cha Ufundi Stadi Ngazi ya 3 (National Vocational Award Level III) au Cheti cha Majaribio ya Ufundi Stadi Daraja la Kwanza (Trade Test Grade One) au sifa linganishi inayotambulika na Mamlaka za Urekebu na Ithibati.

**Muda wa Masomo**

Muda wa masomo kwa kozi hii ni mwaka mmoja (Miezi 12).

**1.3 Mfumo wa Ujifunzaji**

**1.3.1** Kuhudhuria mafunzo kwa njia ya Elimu Masafa na Ujifunzaji Huria (DOeL) kupitia vituo vifuatavyo vya Kanda:

i. Kanda ya Kaskazini-Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Moshi (VETA Moshi).
ii. Kanda ya Ziwa -Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Mwanza (VETA Mwanza)
iii. Kanda ya Kati-Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dodoma (VETA Dodoma).
iv. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini-Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma Cha Mkoa wa Iringa (VETA Iringa)
v. Kanda ya Dar es Salam-Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dar es Salaam (VETA Dar es Salaam).
vi. Kanda ya Magharibi-Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Tabora (VETA Tabora).
vii. Kanda ya Mashariki (Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro-MVTTC)

**1.4 Stashahada ya Uhandisi Ujenzi katika Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi (Ordinary Diploma in Civil and Construction Engineering with Technical and Vocational Teacher Education)–NTA Level 6)**

**Sifa za Kujiunga**

Cheti cha Elimu ya Sekondari (CSEE) chenye ufaulu wa angalau masomo mawili yasiyo ya Dini na Cheti cha Taifa cha Ufundi Stadi (NVA Level Three) Ngazi ya 3 au Cheti cha Majaribio ya Ufundi Stadi Daraja la Kwanza katika Fani Handisi za Ujenzi.

**Au**

Cheti cha Elimu ya Sekondari (CSEE) chenye ufaulu wa angalau masomo manne, mawili kati ya hayo LAZIMA yawe ni miongoni mwa Hisabati, Fizikia/Sayansi ya Handisi, Kemia au Lugha ya Kiingereza au Masomo ya Ufundi kutoka Shule za Sekondari za Ufundi.

**Muda wa Masomo**

Muda wa masomo kwa kozi hii ni Miaka Mitatu (Miezi 36)

## 1.5 Stashahada ya Uhandisi Umeme katika Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi (Ordinary Diploma in Electrical Engineering with Technical and Vocational Teacher Education)–NTA Level 6)

**Sifa za Kijiunga**

Cheti cha Elimu ya Sekondari (CSEE) chenye ufaulu wa angalau masomo mawili yasiyo ya Dini na Cheti cha Taifa cha Ufundi Stadi (NVA) Level Three) Ngazi ya 3 katika Fani Handisi za Umeme zinazotambulika.

**Au**

Cheti cha Elimu ya Sekondari (CSEE) chenye ufaulu wa angalau masomo manne, mawili kati ya hayo LAZIMA yawe miongoni mwa Hisabati, Fizikia/Sayansi Handisi, Kemia, au Lugha ya Kiingereza au Masomo ya Ufundi kutoka shule za ufundi.

**Muda wa Masomo**

Muda wa masomo kwa kozi hii ni Miaka Mitatu (Miezi 36)

### 1.5.1 Mfumo wa Ujifunzaji

Kuhudhuria mafunzo ya Ana kwa Ana Chuoni-MVTTC

**Ada za Mafunzo kwa kila Kozi**

Maelezo zaidi kuhusu muundo wa ada yanapatikana katika tovuti ya chuo www.mvttc.ac.tz.

**2.0. Utaratibu wa Maombi ya Kujiunga na Mafunzo**

Maombi ya kujiunga na mafunzo yanafanywa kwa kujaza fomu inayopatikana kutoka tovuti ya VETA: www.veta.go.tz au MVTTC: www.mvttc.ac.tz kwa gharama ya Shilingi 10,000 tu. Maelezo ya namna ya kupata Namba ya Malipo "Control Number" kwa ajili kulipia fomu yanapatikana kupitia Ofisi ya Uhasibu ya Chuo.

**Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 30 Machi, 2025.**

Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kwa namba **0765191919 au 0682292094.**

**Tangazo hili limetolewa Na;**

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro,
S.L.P. 671, 1 Barabara ya Rwegasore, 67181 Boma, Morogoro CBD
Simu: +255 23 2614466, Nukushi: +255 23 2614466,
Barua Pepe: mvttc@veta.go.tz, Tovuti: www.mvttc.ac.tz.